

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

**Kuhusu Ziara kwa Waziri wa Maswala ya Kidini
(Imetafsiriwa)**

Siku ya Jumanne asubuhi 10/11/2020 M, ujumbe kutoka Hizb ut-Tahrir / Wilayah Tunisia, uliojumuisha Mkuu wa Afisi ya Kiasia, Ustadh Yassin Bin Yahya, Mkuu wa Kamati Kuu ya Mawasiliano, na Ustadh Muhammad Al-Habib Al-Hajjaji, mwanachama wa Kamati Kuu ya Mawasiliano, ulimtembelea Waziri wa Maswala ya Kidini, Bwana Ahmed Adhoum, afisini kwake katika makao makuu ya Wizara hiyo. Kulikuwa na majadiliano naye juu ya suala la kufunga misikiti na msimamo wa Hizb kuhusu hilo. Ujumbe huu wa Hizb ulimbebesha waziri huyo mas'uliya ya kitendo hiki ambacho kinapingana na hukmu za kisheria zinazohusiana na hili, na kumtaka achukue hatua ili kukomesha uhalifu huu mara moja. Ujumbe wa Hizb ulibaini mwingiliano wa waziri na matakwa ya Hizb, ambaye alionyesha utayari wake wa kuondoa marufuku hiyo kama ilivyo katika kikao cha bunge kitakachofanyika Novemba 15.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Tunisia**